

^{Mwafrika} Wananchi 186 wamo 5/8/63 nguvuni Msumbiji

Dar es Salaam, Jumapili.

WANANCHI 186 wametiwa nguvuni na Serikali ya Kireno katika Msumbiji hivi karibuni. Haya yanaelezwa katika taarifa rasmi ya chama cha watoro wa Msumbiji kilichopo Dar es-Salaam, FRELIMO, leo.

Taarifa hiyo inaeleza kwamba kukamatwa kwa jamaa hao kunatokana na "kujitolea kabisa" walikokufanya katika mambo ya siasa ili kudai uhuru wa nchi yao.

Inaelezwa zaidi na taarifa hiyo kwamba jamaa hao waliokamatwa wengine wao walipigwa mpaka wakazimia na kujeruhiwa hata ikabidi kwanzwa wapelekwe hospitalini kutibiwa.

Taarifa ya FRELIMO inazidi kueleza kuwa kuna matumaini machache kwa jamaa hao kupona ama kurudia hali ya maisha yao kama ilivyokuwa zamani, na kwamba wanalindwa katika hali mbaya katika hospitali ya wilaya ya Mueda, katika Jimbo la Cabo-Delgado.

Mbali na jamaa hawa 186, yasema taarifa ya FRELIMO, watu kadha wa kadha hukamatwa kuhusikana na mambo ya siasa na kupelekwa kufungwa katika jela ya mji mkuu wa Msumbiji - Lourenco Marques.

Baada ya kukamatwa kwao, na kabla ya kupelekwa jela, yasema taarifa ya FRELIMO, jamaa hao hupelekwa mbele ya D.C. ambako hupewa ulevi mkali wa kizungu (Cognac) ili kwamba baada ya kulewa husema maneno ovyo kuhusu siri za chama cha FRELIMO.

Alfons